MAHUSIANO YA DOLA NA JAMII YENYE MWAMKO

Na ng'wanza kamata
Idara ya Siasa na Utawala
Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam

1.0 UTANGULIZI

Suala juu ya mahusiano ya Dola na Asasi zisizo za kiserikali si suala jipya, ni suala ambalo limezua mjadala miongoni mwa wanazuoni kwa miaka na miongo mingi iliyopita. Aidha aina ya mahusiano ya dola na asasi hizi nayo yamekuwa, na yametarajiwa kuchukua sura tofauti, ama zinazokubalika au zisizokubalika katika nadharia na itikadi mbalimbali. Leo hii tunapojadilianA juu ya suala hili yapo mawazo mbalimbali, yanayokinzana juu ya mahusiano ya dola na asasi zisizo za kiserikali, nafasi ya asasi zisizo za kiserikali katika kuleta maendeleo, au mabadiriko (inategemea mtu anatazama wapi), au mchango wa asasi hizi katika suala zima la maendeleo na ujenzi wa demokrasia. Ni wazi masuala yote haya kila yaulizwapo hutolewa majibu rahisi au magumu, lakini mara zote majibu yatolewayo hutofautiana na huzaa mjadala mkali.

Hata hivyo jambo moja muhimu linalokosekana katika mijadala mingi, na haswa katika mijadala juu ya nafasi ya dola na asasi zisizo za kiserikali kila moja peke yake na ama kwa uhusiano wake, na nafasi zao katika kufanya nini na ndani ya mfumo upi wa uzalishaji, wa kisiasa na kiutawala. Mara nyingi kwa mfano hatujiulizi ni mfumo upi wa uzalishaji unaotamba katika wakati tulio nao? Katika mfumo huo nani anazalisha mali, nani anafaidika na uzalishaji mali huo, na nani hafaidiki na uzalishaji mali unaofanyika katika mfumo uliopo. Aidha hatujiulizi ni mfumo gani wa mawazo (itikadi) unaoongoza na kuhalalisha mfumo wa uzalishaji uliopo, na ni asasi zipi zinazosaidia kuhanikiza au kuwa mwega wa mfumo huo wa uzalishaji. Tunachokusudia kusema hapa ni kuwa dola au asasi za kiserikali zaweza, katika mfumo wa uzalishaji unaotamba, vikajikuta vikifanya kazi moja au mbalimbali lakini zenye lengo moja, lile la kuuendeleza na kuuhalalisha mfumo huo, au zikafanya kazi tofauti zenye malengo tofauti kimoja kikitaka kuuendeleza mfumo na kingine kikipigana kuubadilisha mfumo. Ni shabaha yetu kujadili mahusiana ya dola na asasi zisizo za kiserikali katika mfumo uliopo na unaotamba hivi

sasa hapa nchini na sehemu nyingi za dunia – uchumi wa soko, yaani *ubepari wa kitandawazi.*

2.0 MIFUMO YA UZALISHAJI, DOLA NA ASASI ZISIZO ZA KISERIKALI

Wakati nafikiria nini cha kuandika juu ya mada hii, jambo moja lilinijia akilini, nalo ni mahusiano ya wamisionari wa kikristo na dola la kikoloni. Simulizi nyingi za ujio wa wakoloni katika bara la Afrika zinaeleza kwamba mashirika mbalimbali ya kidini yalituma watu wao katika bara la Afrika kwa ajili ya kueneza ustaarabu wa kimagharibi, ikiwemo dini ya kikiristo na kufanya biashara. Watu maarufu waliobeba sifa hizo ni pamoja na David Livingstone ambaye alizifanya kazi hizo kwa ustadi na dhati kubwa. Lakini, historia pia inatueleza, kuwa kila walikopita wamisionari basi makampuni ya biashara na uzalishaji toka ulaya yalifuata au kuambatana na wamisionari hawa, na baadaye ukoloni ukajikita na dola na mfumo wa kikoloni ukaanzishwa. Ukoloni kama mfumo wa uzalishaji ulianzishwa kwa mabavu (kwa sababu watu walipinga) ukahalalishwa kwa imani na madai ya kuwastaarabisha waafrika. Kazi ya dola hapa ilikuwa ni kutengeneza sheria, kanuni na taratibu mbalimbali ambazo zingewezesha malengo ya ukoloni kufanikiwa, lakini pia kuandaa na kuweka askari na vikosi kwa ajiri ya kuwaburuza kwa mabavu watawaliwa pale hiari iliposhindikana. Aidha, asasi zisizo za kiserikali, kama mashirika mbalimbali ya dini nayo yalitoa mchango wake ule wa kuuhalalisha mfumu ule dharimu, uliojaa dhuruma, ukandamizaji na unyanyasaji. Wao wakihubiiri upendo, utii na uvumilivu, na heri atakayoipata aliye mtii, na mvumilivu, masikini na fukara baada ya kifo; na kuwaacha wanyonyaji wa kizungu wakipora rasilimali na kuutweza utu wa waafrika. Nachosema hapa ni kuwa dola na dini (kama asasi isiyo ya kiserikali kwa Mtazamo wa mwanamapinduzi msomi wa Kitaliano Antoni Gramsci) kwa mfano huu wa mfumo wa uzalishaji wa kikoloni vilifanya kazi tofauti lakini zenye lengo moja, la kuanzisha, kusimamisha na kuendeleza na kuhalalisha mfumo ule.[1]

[1] "The Christian Missionaries were as much part of the colonizing forces as were the explorers, traders, and soldiers. …. But there is no doubting the fact that missionaries were agents of colonialism in the practical sense" (Tazama Walter Rodney: *How Europe Underdeveloped Africa*. East African Educational Publishers; Nairobi, 1982. p. 252.

Ni wazi kwamba ukoloni ulishinda na kutawala waafrika, lakini hili lilikua ni jambo la muda tu kwani waafrika waliendelea kupinga ukoloni, na vuguvugu jipya likazaliwa, vuguvugu lenye kutaka kumaliza ukoloni na mfumo wake wa uzalishaji mali. Katika Afrika mashariki, ukiacha vyama vya siasa ambavyo vingi vilikuja kuundwa baada ya mwaka 1950, vipo vikundi vingi na vilabu vingi vilivyoanzishwa kwa malengo mbalimbali, na hata vilipoanzishwa vyama vya wafanyakazi na vyama vya ushirika Vugu vugu la kudai uhuru lilipata nguvu kubwa. Vuguvugu lililozaliwa wakati huu lilitokana na makundi mbalimbali ya wanajamii waliojijumuisha kwa sura mbalimbali na malengo mbalimbali. Kilichokuwa kikiwaleta pamoja katika mchakato huo ni utawala na mfumo wa kikoloni uliowadhalilisha, kuwanyonya na kuwakandamiza wao wote kama waafrika. Wafuasi wa Vuguvugu hili la uhuru walikuwa ni watu wa tabaka tofauti, wenye nafasi tofauti katika mfumo wa uzalishaji na unyonyaji wa kikoloni. Katika zama hizo za harakati za ukombozi, aina ya asasi zisizo za kiserikali zilizoanzishwa hasa na waafrika zilichochewa na haja ya kupambana na ukoloni na kuondosha mfumo ule. Kwa hivyo mahusiano ya asasi hizi na dola yalikuwa yenye ukinzani kwa sabau malengo yao katika mfumo uliopo yalitofautiana. Dola la kikoloni likitaka kuendeleza mfumo na asasi zisizo za kiserikali zikitaka na kupambana kuuangusha mfumo huo.

Nisingependa kuingia katika mjadala wa nini kilitokea wakati wa uhuru na nini ilikuwa nafasi ya asasi zisizo za kiserikali na zilikuwa na mahusiano gani na dola. Tuseme kwa ufupi tu kwamba katika nchi zote za Afrika Mashariki, kama ilivyokuwa katika sehemu kubwa ya Afrika, suala la kujumuika nje ya dola na vyombo au asasi zake lilikuwa ni gumu kwa sababu ya aina ya tawala zilizotokea. Lakini hatuwezi kusema kabisa kwamba hakukuwa na asasi zisizo za kiserikali, zile zilizokuwepo kazi na malengo yake hayakutofautiana nay ale ya dola, na zile zote ambazo zilikuwa zina malengo au kuashiria kutofautiana na dola kimalengo vilifishwa na kupigwa marufuku. Kwa kiasi kikubwa asasi huru zisizo za kiraia zilitoweka katika ramani ya siasa za Afrika, au kuendesha harakati za chini kwa chini.

3.0 DOLA NA ASAZE NDANI YA MFUMO WA UCHUMI WA SOKA

Mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa katika bara la Afrika hususan hapa Afrika Mashariki kuliambatana na uanzishaji wa mfumo wa kisiasa na kiuchumi unaoongozwa na nadharia na itikadi ya *kiliberali-mamboleo.* Itikadi na dhana hii inasisitiza sana suala la uhuru wa mtu binafsi – uhuru wa kuzungumza, kujishirikisha, na kuchagua miongoni mwa mambo mengine. Kazi ya dola la kiliberali, angalau kwa nadharia ni kuhakikisha kuwa uhuru huu wa mtu binafsi unalindwa kwa kila hali. Dhana na itikadi ya kiliberali inaamini kuwepo kwa umiliki wa mali binafsi na ushindani katika soko. Itikadi na dhana hii inaamini kuwa umasikini unaweza kutokomezwa kwa njia ya ushindani katika soko na msukumo na tamaa ya kila mtu kujipatia na inapowezekana kujilimbikizia mali. Umasikini na utajiri, kwa mujibu wa dhana na itikadi hii hautokani na mahusiana katika uzalishaji, kwamba kuna anayezalisha (anayeishia kuwa masikini) na kuna anayenyonya (anayekuwa tajiri). Umasikini ni tokeo la kutokuwa mjasilimali mzuri, kwa kutojua wapi uwekeze, na kutokuwa mbunifu na mchapa kazi kwa bidii.

Lakini ni wazi kuwa mfumo huu ni wa kibepari, ambao msingi wake ni *uporaji* na *upokaji* wa mali za walio wengi – wazalishaji mashambani na viwandani. Hapa katika mazingira yetu tunawakusudia wakulima wa vijijini na wafanyakazi. Chini ya mfumo wa uchumi wa soko mali na rasilimali za wanyonge zinapokwa – ardhi, madini, na mali asili zingine. Lakini nguvu na jasho lao linaporwa kwa njia za soko holela ambalo linatumika kuwapora huku dola la kiliberali likihalalisha kutofanya chochote[2] kwa madai kuwa hili ni soko hulia. Wafanyakazi pamoja na kuwa na vyama vyao vya wafanyakazi lakini kwa kuwa tuko katika mfumo wa uchumi wa soko, ni vyema kila mfanyakazi awe na uhuru wa kuchagua mwajiri na kutobanwa kuwa kwa mwajiri mmoja – uhuru wa kuchagua, na matokeo yake ni sheria na mikataba ya kazi kama ile ya manamba. Kimantiki hizi ni taratibu zinazoua umoja na mshikamano baina ya wafanyakazi na kumrahishia mnyonyaji fursa ya kunyonya. Aidha, kwa mantiki hiyo hiyo ardhi ya wakulima maskini lazima itambuliwe kwa ama kupewa cheti (kama kile cha MKURABITA kwa hapa Tanzania) au kwa hati miliki. Lengo ni kujenga mahusiano ya ardhi ya mtu na mtu na sio

[2] Nyakati zingine hujifanya linafanya chochote, na hasa kupitia matamshi ya kisiasa ya viongozi, lakini huwaacha wakulima kuendelea kunyonywa na wafanyabiashara wenye baraka za Serikali.

jumuia/ukoo. Miliki ya jumla inayohusisha watu wengi inajenga msingi wa kujenga umoja na mshikamano katika kupinga uporaji wa rasilimali hizo. Hoja inayotolewa ni kuwa mtindo huu utawaongezea zaidi wamiliki wa ardhi na rasilimali hizo uhakika wa miliki na wataweza kujipatia mikopo ili kupunguza umasikini.

Tunachotaka kusema hapa ni kuwa dola katika mfumo wa kiliberali-mamboleo, kama lilivyokuwa dola la kikoloni linayo kazi moja kubwa kujenga na kutengeneza mazingira yatakayofanya mfumo wa uzalishaji na umiliki mali wa kinyonyaji kufanya kazi bila kipingamizi. Mfumo wa kiliberali, pamoja na uhuru wa mtu binafsi unataka utawala wa sheria. Kwa tafsiri yangu, kila kitu kinatakiwa kifanyike na kionekane kimefanyika kwa njia zinazokubalika kisheria – kwa maneno mengine wizi na uporaji unafanyika na kuhalalishwa kwa mujibu wa sheria. Lakini sura ya dola inajitokeza wazi sio tu katika aina ya sheria inazotunga – zinazoruhusu upokaji wa mali na rasilimali za wanyonge kama vile huduma za jamii (elimu na afya ambazo zikitolewa na kupatikana kwa kulipiwa na dola) bali pia kwa jinsi dola linavyopendelea wazi wazi upande wa wanaoitwa ‘wawekezaji’ na makampuni ya kimataifa na taasisi za kimataifa za kukuza na kuendeleza mfumo huu (kama vile Benki ya Dunia na I.M.F.) dhidi ya maslahi ya wakulima na wafanyakazi, na ‘wajasilimali’ wa ndani kama vile wamachinga wa Tanzania. Unapotokea mgogoro baina ya wafanyakazi na mwajiri wao (Kampuni binafsi) dola itaingilia kwa upande wa tajiri, na inapotokea kuna mgogoro baina ya wakulima na mporaji ardhi dola likiingilia mara nyingi litaingilia upande wa waporaji. Hata ulinzi na usalama unaimarishwa na unahakikishwa zaidi katika mali na rasilimali za matajiri na maeneo wanayoishi – na sio wanakoishi wanyonge.

Katika sura hii ya dola nini nafasi ya asasi zisizo za kiserikali na nini mahusiano yake na dola? Kwanza, ni wazi kuwa ndani ya mfumo wa uchumi wa soko asasi zisizo za kiserikali zilizozoeleka huko nyuma na kuleta upinzani mkubwa na waajiri na dola – vyama vya wafanyakazi na ushirika wa wazalishaji umedhoofishwa. Ni tokeo la mfumo wenyewe. Badala yake kumezaliwa aina mpya ya mijumuiko, ambayo sura na sirika yake haifanani kabisa na vyama vya wafanyakazi na ushirika wa wazalishaji.

Vyama vya wafanyakazi na ushirika wa wazalishaji – wakulima ni vyama vya kitabaka. Matabaka ya wazalishaji yakijumuika yakiwa na malengo yenye maslahi kwa tabaka linalohusika. Madai yao, mapambano yao pamoja na sura zake tofauti, yalikuwa ni madai na mapambano ya kitabaka. Wafanyakaki wakitaka sehemu kubwa zaidi ya jasho lao na kupunguza ziada ya mwajiri, na wakulima wakidai na kutafuta sehemu kubwa zaidi ya jasho lao kutokana na mazao yao. Vyama hivi vilikuwa vina wanachama na uongozi uliochaguliwa. Vyama hivi katika mapambano yake vingeweza kufika mahala, na historia inatwambia vilifika hapo, vikaona faida ya kuachana na mfumo wa uzalishaji uliopo na kuanzisha mfumo mwingine wenye maslahi makubwa kwa wazalishaji. Kwa maneno mengine vyama hivi vilikuwa ni sehemu kubwa ya fikra za siasa za *kiukombozi*.

ASAZE za leo ndani ya mfumo wa soko zina sura tofauti. Nyingi zinaanzishwa na wateule (elite), kitabaka hawana tofauti na wale walioshikilia dola. Ziko mijini, na hazina sura za kitabaka kama ilivyo kwa vyama vya wafanyakazi na wakulima. Malengo yake ni ya ama kurekebisha mambo au mahusiano baina ya makundi ya watu – sio ya kitabaka, au kuwahurumia na kuwasaidia watu wenye shida – kama vile watoto yatima, wenye ulemavu, au kwa lugha ya kiliberali – kuwawezesha vijana/wanawake n.k. ili wajikwamue na umasikini. Zingine zinaelimisha wananchi habari ya demokrasia na jinsi mfumo wa vyama vingi unavyotakiwa kufanya kazi na jinsi wao wanavyoweza kushiriki katika mfumo huo, na wengine wakichukua sehemu moja au nyingine ya masuala yanayohusiana na haki – haki za binaadamu, haki za watoto na ukomeshaji wa ajira za watoto n.k. Katika sura hii ya ASAZE nini yatakuwa mahusiano yake na dola?

4.0 ‘WADAU’ AU WAKINZANI KATIKA MABADILIKO?

Wapo wanazuoni ambao wanaamini kuwa dola na jamii (civil society) ni vitu viwili vinavyoweza kutenganishwa. Na katika utenganisho huo nafasi ya *civil society* ni kutoa upinzani kwa dola, kwa maneno mmengine na hasa katika mfumo wa soko upinzani wa kweli kwa dola utatoka kwa civil society. Aidha, kwenye dhana hii hii wapo wanaodhani kuwa kazi ya ASAZE ni kuikosoa, kuiamsha, kuielekeza na kuiwajibisha dola. Kutokana na dhana hii mahusiano ya dola yatakuwa ni yale ya kupingana na kukinzana na wala si ya ‘KIDAU’.

Aidha kuna wanazuoni ambao wanaiangalia dhana ya mahusiano ya dola na *civil society* kwa mtazamo tofauti. Wao wandhani kuwa utenganisho wa *dola na civil society* ni suala lisilo na ushahidi wa wazi katika historia. Wao wanaamini kuwa upo umoja wa dola na *civil society* umoja ambao unazaa kile kinachoitwa *hegemony.* Katika muunganiko wa aina hii lengo la dola na ASAZE linakuwa ni moja kulinda dola na mfumo wa uzalishaji uliopo. Dola ikitumia uhodhi wake wa matumizi ya nguvu na ASAZE zikifanya kazi ya kuhalalisha dola na mfumo kwa njia za kiitikadi, imani, na maadili na utamaduni. Ndio maana katika dhana ya ASAZE katika fikra hizi asasi za kidini, asasi za elimu kama vyuo vikuu, vyama vya wafanyakazi, familia, n.k vyote vinafanya kazi moja ya kufanya mfumo wa mawazo unaohimili mfumo ukubalike na kila mtu na uchukuliwa kama ulivyo bila kuhojiwa (kuunda kinachoitwa *common sense*). Mfano wa umoja baina ya dini na dola wakati wa kuanzishwa na kuendelezwa kwa ukoloni barani afrika tulioutoa awali unaakisi hali hii kwa nyakati zilizopita. Mtazamo wa wanazuoni wa kundi la mwanzo, wanaoona ASAZE kama kinzani wa dola, unafikiriwa pia katika mtazamo huu lakini hali hiyo itatokea tama kutakuwa na Vuguvugu lenye mtazamo na malengo tofauti – yale ya kuudodosha mfumo uliopo *(counter hegemony).* Hali kama hii kwa mawazo yangu ilijitokeza wakati wa harakati za uhuru barani Afrika.

Je, kwa hali ilivyo leo hii ASAZE zetu zinafanya kazi gani? Na katika kazi hizo zinajenga mahusiano gani na dola na zinatoa mchango gani katika kujenga misingi ya mabadiriko au mwendelezo wa mfumo uliopo?

Kujibu maswali haya ningependa kubainisha kazi nne za ASAZE ambazo ni *umisionari, umamluki, wakombozi, wanamapinduzi?*[3]

Kazi ya ***wamisionari*** wakati wa ukoloni haikuishia tu katika kueneza injili na ustaarabu mpya bali pia iliambatana na kutoa ‘misaada mbalimbali kwa ajili ya kile kilichoitwa maendeleo ya watu. Kilichosukuma hali hiyo anaandika Manji na O’Coill, ni haja ya

[3] Maneno haya nimeyakopa toka kwa Prof. Shivji, japo katika tafsiri kwa ajili ya mada hii yaweza kuwa na maana tofauti na ile aliyokusudia Prof. Shivji.

kuulinda mfumo lakini wa woga wa mapinduzi dhidi ya mfumo – kwa hivyo mashirika ya kidini na mengine yalitaka kuonesha wema na kujali kwa kutoa misaada na vitu mbalimbali kwa masikini. Kwa maneno mengine wamisionari wakifanya, pamoja na mambo mengine jitihada za kuwapoza masikini na wanaooteswa kwa kuwapa matumaini ili wajiepushe na hasira zitakazowasukuma kujiunga na harakati za kuuangusha mfumo wa ukoloni. Leo kwa maoni ynagu tunazo ASAZE ambazo kwa 'mioyo' yao ya huruma, na nia njema zao zinasaidia kuuimarisha mfumo – kwa kutoa dhana kuwa kama kuna mtu au ASAZE yenye kuonyesha huruma basi tatizo haliwezi kuwa kwenye mfumo bali uchache wa watu wenye huruma. Uhusiano wa ASAZE ya aina hii na dola hautakuwa wa kukinzana utakuwa uhusiano wa KIDAU kwa sababu wote wanafanya kazi zenye lengo moja, kuulinda mfumo.

Dhana ya ***umamluki*** ni dhana ambayo imetumika sana katika yale yanayoitwa 'majeshi ya kukodiwa'. Watu ambao wanaajiriwa kwenda kupigana vita katika nchi nyingine, lengo lao likiwa ni malipo baada ya kukamilisha kazi yao. Hawana maslahi mengine zaidi ya malipo.[4] Katika dunia ya leo ambamo mfumo mkuu ni ule wa *kiliberali-mamboleo*, ambao kidunia unaelezwa na kutetewa kama utandawazi, wapo watu na ASAZE ambazo zimejikuta; kwa kujua au kutojua, au kutojali au kutaka kujua, zikifanya kkazi ya kimamluki. Kwamba kazi zao ni kueneza mawazo na kutetea mipango toka nje ya nchi zao na kuipigia debe ili ikubalike wakati mawazo na mipango hiyo ni sumu na ina madhara makubwa kwa wananchi wenzano. Lakini wao hupofushwa na manufaa kidogo wayapatayo, kama ilivuyo kwa mamluki, kutokana na misaada waipatayo kwa ajili ya kufanya kazi hizo. Kama dola pia ni la kiliberali au linashabikia mipango ya aina hiyo, kama ilivyo sasa katika nchi zetu basi kunaweza kusiwe na mahusiano mabaya. Lakini hutokea hawa mamluki wakatumika kuidhoofisha dola kwa maslahi ya wanaowatumia, pale dola inapujisikia kusukumwa sana basi hugeuka na kukemea ASAZE za aina hizo. Mifano mizuri tunaweza kuiona katika matukio ya ASAZE zinazokema masuala ya kukosekana kwa utawala bora na ufisadi. Kimsingi, ajenda ya ufisadi au utawala bora – kwa namna inavyojadiliwa hailengi kuubadili mfumo.

[4] Tofauti ya umamluki yaweza kuwa uzalendo, majeshi katika historia ya dola za kisasa huundwa na wananchi na hao hupigana sio kwa sababu ya malipo, wako tayari kufa kwa ajili ya kulinda nchi, taifa, na dola yao, ambayo kwayo wanatoa utii wao.

Dhana ya ***wakombozi*** inalenga kwenye ASAZE ambazo mbele za umma na watu 'zinaowalenga' kuwa zinawapelekea ukombozi. Ukombozi unaokusudiwa ni ule unaojitokeza katika sura mbili ya kwanza ile ya kuwasemea watu na ya pili ni ile ya kuwawezesha watu. Sura hizi mbili zimejengwa juu ya fikra kwamba watu hawawezi kujisemea wenyewe na kama itabidi wajisemee wenyewe basi hapana budi kuwaelimisha (some kuwawezesha). Hizi zinafanywa sana na ASAZE za uragbishi, ushawishi na uzengeaji. Mara zote ASAZE za aina hii zimelenga katika kushawishi mabadiriko ya sera na sheria aghalabu bila ushiriki wa moja kwa moja ya wale wanaosemewa/kuwakilishwa. Mahusiano ya dola na ASAZE zinazofanya kazi za aina hii yanaweza yakaleta mkwaruzano kidogo japo sio mara zote na ni rahisi kwa dola kutoa fursa (ushirikishwaji) kwa ASAZE za aina hii katika kamati za maamuzi na kuzinyamazisha, au kuzidhoofisha zisiendeleze kazi ya upayukaji unaoweza kuamsha hasira za watu.

Kutokana na kazi hizi hakuna tishio kubwa sana kwa dola na mfumo. Kwa njia moja ASAZE, kwa kazi za kimisionari, kimamluki, au zile za wakombozi zinasaidia kupoza hasira za wanyonge kwa ama kuwapa matumaini ya maisha bora – kwa kuwafundisha ujasiri mali, namna ya kurasmisha mali zao, namna ya kuandika michanganuo ya miradi. Aidha ASAZE zinausaidia mfumo na dola kwa kuwapa matumaini watu kuwa wasiwe na wasiwasi kwa sababu wapo watu au ASAZE ambazo zinashughulikia mambo yao. Kwa mwongozo wa mtazamo wa ki-Gramsci nadiriki kusema, pamoja na mchango wa ASAZE katika jamii, kazi kubwa zinazofanya zinasaidia sana kujenga ***common sense***, yaani kuufanya umma uupokee nakuubali mfumo wa soko – yaani unyonywaji na ukandamizwaji wao bila kufurukuta.

5.0 HITIMISHO: MAPAMBANO YA WANUYONGE NA ASASI ZA KIMAPINDUZI

Kwa baadhi ya wanazuoni wakosoaji wa mfumo wa uchumi wa soko ***uliberali-mamboleo*** ni mfumo wa mpito, ahadi zake za uhuru wa watu na dola lisiloingilia soko linaloruhusu ushindani vinakinzana na maslahi ya tabaka linalofaidika. Kutokana na upinzani dhidi ya mfumo huu, unaosababishwa na sababu zilizo dhahiri, ufukarishaji

unaotokana na upokaji wa mali za walio wengi, dola linajikuta likilazimika kutumia mabavu kuzimisha upinzania wa watu. Katika sehemu mbalimbali za nchi zetu watu hawajakaa na kuridhika na jinsi mambo yanavyokwenda, kwa namna mbalimbali wamelalamika na kutoa upinzani, pale walipoweza dhidi ya uporaji na upokaji wa mali zao. Wafanyakazi, pamoja na kudhoofishwa kwa vyama vyao bado wamepambana na waajiri wao. Lakini zi wapi sauti na ushiriki wa ASAZE zisizo za kiserikali katika mapambano haya. Majibu tunayo, lakini mara nyingi tuko maofisini tukikamilisha taarifa za kupeleka kwa ‘wafadhili’ ili tusije kukosa fedha kwa ajili ya kuendeleza kazi zetu, au tuko ofisi za serikali tukizengea, kuomba fursa ya kushiriki katika kamati za mamauzi au kupitia sera. Hatujatumwa na watu tumejituma wenyewe, hatuwajibiki kwa watu ila kwa wenyewe na wanaotupatia fedha. Kwa vile tunaowasiliana nao na kupenda kushirikiana nao ni wateule wenzetu mahusiano yetu na wao (dola) ni ya KIDAU zaidi. Mahusiano yanayojengwa kwenye taswira hii hayana malengo yenye kuleta tumaini la ukombozi wa wanyonge. Kuna haja ya kutafakari vizuri na kwa makini zaidi aina na mjumuiko na organizesheni zinazoweza kuunganisha mapambano ya wazalishaji wa aina mbalimbali ili kujenga nguvu ya pamoja kwa ajili ya ukombozi wao. Ni wazi, mahusiano ya asasi za namna hiyo, zenye kuhoji mfumo uliopo na nafasi ya dola katika mfumo huo zitakuwa na ukinzani mkubwa na dola. Kwa sababu zitakuwa zinalenga katika kuuangusha mfumo huo. Asasi za namna hiyo kwa sasa hazipo katika eneo letu hili la Afrika mashariki.